mjasiriamali @mjasiriamali @mjasiriamali

# MJASIRIAMALI

KAMATA FURSA

Tovuti www.smjasiriamali.co.tz/ISSN 3456-1679 Na. 39, Jumatano Machi 5, 2025 Bei Tsh. 1000/=Ksh 100

## TANGA YAFUNGUKA...

# Maono ya Rais Samia kutimizwa



- WAAHIDI KUENDELEA KUTEKELEZA MAONO YAKE ALIYOYATOA KWAO
- HII NI KATIKA KUFUFUA VIWANDA, KUBORESHA MIUNDOMBINU
- WANANCHI WATAKIWA KUUNGA MKONO JUHUDI HIZO

> "Akizungumza mara baada ya ziara ya Rais Dkt. Samia mkoani humo, Balozi Dkt. Batilda amewashukuru wakazi wa Tanga kwa mapokezi mazuri waliyompatia kiongozi huyo wa nchi na kuahidi wataendelea kusimamia kikamilifu fedha za miradi ya maendeleo ili kuhakikisha zinaleta manufaa kwa wananchi.

## UNAFUGA KONDOO? ZALISHA CHOTARA



## Unataka kukopa Benki? njia hizi hapa

# Majaliwa anena juu ya Sekta ya Fedha

NA MWANDISHI WETU

**WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amesema kuwa huduma jumuishi za kifedha ni kiungo muhimu cha ukuaji wa uchumi, kupunguza umasikini na kuchochea maendeleo ya jamii kwa ujumla.**

Amesema Serikali kwa kutambua hilo imedhamiria kuendelea kushirikiana na wadau wote ili kuhakikisha sekta ya kifedha inazidi kuwa jumuishi, fanisi, na yenye tija kwa maendeleo ya Taifa.

Amesema hayo juzi alipozindua huduma mpya za kidijitali za Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) katika ukumbi wa Super Dome, Masaki jijini Dar es Salaam.

Ameongeza kuwa katika vipindi tofauti, Serikali imekuwa ikiandaa na kutekeleza mikakati ya Taifa ya kuboresha huduma jumuishi za kifedha.

“Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa 2023 - 2028 ni mwendelezo wa mafanikio yaliyopatikana kupitia Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha uliokamilika Desemba 2022”

Majaliwa alisema kuwa, jitihada nyingine ni kuandaa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa miaka 10 kuanzia mwaka 2024 hadi 2034.

“Mkakati huu umeainisha malengo mahsusi ambayo kama nchi tunaazimia kuyatekeleza ili kufikia uchumi wa kidijitali.”

Kwa upande wake, Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Sauda Msemo amesema sekta ya fedha imeendelea kuwa na ustahimilivu na hivyo kuwezesha shughuli mbalimbali za kiuchumi kufanyika.

Aidha, Naibu Gavana huyo ametoa wito kwa taasisi zote za kifedha zifuate viwango bora vya usalama wa mitandao na kugundua haraka pale panapotokea udanganyifu wa aina yoyote.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi alisema lengo la uzinduzi wa huduma hizo za NBC kidijitali ni kuboresha utoaji wa huduma za kifedha na kuzifanya zipatikane kwa urahisi. “Huduma hizo ni pamoja na ufunguaji wa akaunti, kuhamisha fedha, kupata mikopo bila ya kwenda katika tawi.”

# TAMISEMI yajiweka sawa Bima ya Afya

NA MWANDISHI WETU

**MKURUGENZI wa Idara ya Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dkt. Rashid Mfaume, amesema kuwa katika kuelekea utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, TAMISEMI imejipanga vyema kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora huduma za afya katika ngazi ya msingi.**

Dkt. Mfaume ametoa kauli hiyo alipokuwa katika ziara yake ya kukagua utoaji wa huduma za afya, lishe, na ustawi wa jamii mkoani Dodoma, ambapo alitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

Amesema TAMISEMI itahakikisha katika ngazi ya afya ya msingi bidhaa zote muhimu za afya zinapatikana.

"Tunawahakikishia Watanzania kuwa katika ngazi ya huduma za afya ya msingi, Ofisi ya Rais TAMISEMI imejipanga kuhakikisha wananchi wote wanaojiunga na Bima ya Afya kwa Wote wanapata huduma zote stahiki kama inavyotakiwa," amesema Dkt. Mfaume.

Aidha, amebainisha kuwa hapo awali kulikuwapo na changamoto ya baadhi ya wanachama wa bima ya afya kukosa dawa katika vituo vya kutolea huduma na kulazimika kununua dawa hizo wenyewe.

Hata hivyo, kwa sasa TAMISEMI imechukua hatua kuhakikisha vituo vya afya vinakuwa na akiba ya kutosha ya dawa na vifaa tiba ili kuboresha huduma kwa wananchi.

## Wajasiriamali wapewa elimu ya mikopo

NA ALBANO MIDELO, Songea

**WANA vikundi vya wajasiriamali na wafanyabiashara waliokidhi vigezo vya kupata mkopo wa asilimia kumi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma wamepatiwa mafunzo ya mwisho kabla ya kupokea mikopo hiyo.**

Mafunzo hayo yalifanyika katika ukumbi wa Klasta Mlingoti, mjini Tunduru yakiwa na lengo la kuwaandaa wanufaika kwa matumizi sahihi ya mikopo ili kukuza biashara zao.

Mada zilizofundishwa zilihusisha usimamizi wa fedha, uandishi wa mipango ya biashara, mbinu mbalimbali za kibiashara, na umuhimu wa kurejesha mikopo kwa wakati.

Mkuu wa Kitengo cha Maendeleo ya Jamii katika halmashauri hiyo, Jeceline Mganga, aliwasisitiza wanufaika kutumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa ili waweze kupata faida na kurejesha mikopo bila usumbufu.

“Unaporejesha kwa wakati, unajiongezea sifa ya kukopa zaidi,mikopo ii haina riba, hivyo ni fursa ya kipekee kwa wajasiriamali kuhakikisha inawanufaisha.”,alisema Jakline

Baada ya mafunzo, wanufaika walitakiwa kusaini mikataba ili kukamilisha hatua muhimu ya upatikanaji wa mikopo hiyo. Zoezi hilo lilisimamiwa na Mwanasheria wa Halmashauri, Mwanaharusi Chiutila.

Mikopo hii inalenga kuwawezesha wananchi wa Tunduru kujikwamua kiuchumi, kukuza biashara, na kuchochea maendeleo ya kiuchumi wilayani humo.



# Maono ya Rais Samia kutimizwa

NA MWANDISHI WETU

**MKUU wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dkt. Batilda Burian, amesema wataendelea kutekeleza maono ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuhakikisha maendeleo ya mkoa huo yanaimarika, hususani katika kufufua viwanda na kuboresha miundombinu ya barabara.**

Akizungumza mara baada ya ziara ya Rais Dkt. Samia mkoani humo, Balozi Dkt. Batilda amewashukuru wakazi wa Tanga kwa mapokezi mazuri waliyompatia kiongozi huyo wa nchi na kuahidi wataendelea kusimamia kikamilifu fedha za miradi ya maendeleo ili kuhakikisha zinaleta manufaa kwa wananchi.

“Tutaendelea kuimarisha maendeleo ya Mkoa wa Tanga kwa kuhakikisha rasilimali zinazotolewa na serikali zinatumika ipasavyo. Tanga ina historia kubwa ya viwanda, na jitihada za serikali ni kuirejesha katika nafasi yake kama kitovu cha viwanda nchini,” alisema Dkt. Batilda.

Aliongeza kuwa serikali imejipanga kuboresha mitandao ya barabara ili kuwezesha urahisi wa usafirishaji wa bidhaa na kuinua uchumi wa mkoa huo. Wananchi wametakiwa kuunga mkono juhudi hizo kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo zinazotekelezwa na serikali.

Katika ziara yake mkoani humo, Rais Dkt. Samia ameeleza dhamira yake ya kuhakikisha Mkoa wa Tanga unakuwa pia mkoa wa utalii na kuwa unanufaika zaidi na fursa zitokanazo na fukwe, historia na tamaduni mbalimbali ndani ya mkoa huo.

Akizungumzia ziara yake ya wiki moja katika Mkoa wa Tanga, Rais Dkt. Samia alitoa rai kwa wananchi kutumia ipasavyo fursa za maendeleo zitokanazo na miradi mbalimbali na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ndani ya Mkoa wa Tanga.

Aidha, ametoa rai kwa wananchi kuhakikisha vijana wanapata ujuzi na stadi stahiki ikiwemo kupitia shule, vyuo vya VETA viliyojengwa katika kila wilaya, Chuo cha Mafunzo ya Amali cha Mkoa na kampasi ya Chuo Kikuu Mzumbe kinachotarajiwa kujengwa katika Wilaya ya Mkinga, ili waweze kunufaika zaidi na miradi mbalimbali inayofanyika katika mkoa huo.

# Pindi Chana: Tumedhibiti ujangili

NA MWANDISHI WETU, Dodoma

**WAZIRI wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana ameeleza kuwa wizara imeweza kudhibiti shughuli za ujangili katika maeneo yaliyohifadhiwa na kupelekea ongezeko la idadi ya wanyamapori ikiwemo Tembo, Simba, Chui na Nyati.**

Balozi Dkt. Chana ameyasema hayo katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanyamapori Duniani, yaliyofanyika katika Viwanja vya Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, Dodoma juzi, ambapo alipongeza taasisi zote zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuendelea kusimamia maeneo yaliyo hifadhiwa na kupambana na ujangili.

“Nchi yetu inaongoza kwa idadi kubwa ya wanyamapori, tunayo idadi kubwa ya Simba, Chui, Nyati na niseme kwamba Tanzania ni ya tatu kwa kuwa na idadi kubwa ya Tembo Duniani,” aliongeza Balozi Dkt. Chana.

Naye, Mkurugenzi wa Wanyamapori Tanzania, Dkt. Allex Lobora alieleza umuhimu wa kuadhimisha siku hiyo ambapo inaikumbusha jamii kulinda na kuhifadhi maliasili zetu ikiwemo wanyamapori na mimea iliyopo hatarini kutoweka, kupunguza uharibifu wa mazingira na kuzuia ujangili.

Dkt. Lobora aliongeza “ Siku hii inatoa fursa ya kuonyesha mchango wa wanyamapori katika maisha ya binadamu pamoja na kuhamasisha hatua za kulinda wanyamapori kwa manufaa ya vizazi vijavyo”

Aidha, kaulimbiu ya maadhimisho hayo inasema “Wanyamapori na Uwekezaji Kifedha, Wekeza kwa Watu na Dunia” huku ikihimiza kuwa na mifumo na mikakati endelevu ya kupata na kusimamia matumizi ya rasilimali ili kufikia lengo la uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori.

Maadhimisho hayo yalitanguliwa na maandamano ya amani kutoka Ofisi za Wizara ya Maliasili na Utalii Swagaswaga kuelekea Viwanja vya Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, Dodoma ambapo Balozi Dkt. Chana alitembelea mabanda yaliyokuwa yakitoa taarifa kuhusu elimu uhifadhi wa utalii.

# Utafiti wa madini washika kasi

NA MWANDISHI WETU

**NAIBU Waziri wa Madini Dkt. Steven Kiruswa amekutana na Balozi wa Jamhuri ya Watu wa China nchini Chen Mingjian katika kikao kilicholenga kujadili fursa na maeneo mbalimbali ya ushirikiano katika Sekta ya Madini ikiwa ni mwendelezo wa mazungumzo kati ya Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango na kiongozi huyo .**

Katika mazungumzo yao, Dkt. Mpango aliiomba Serikali ya China kupitia balozi huyo kusaidia shughuli za utafiti wa madini Tanzania, ambapo baada ya mazungumzo yao, Serikali ya China imetuma wataalam wawili kutoka Taasisi ya Jiolojia na Utafiti ya nchini humo ili kufuatilia na kujua mahitaji ya utafiti na maeneo mengine ya mashirikiano kati ya Tanzania na China

‘‘Kikao nilichokiongoza kimejadili maeneo ya ushirikiano na sisi kwa upande wetu tumeweza kubaini maeneo matatu muhimu ambayo Serikali ya china inaweza kutusaidia katika shughuli za utafiti na kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara kulingana na mahitaji,” amesema Dkt. Kiruswa.

Maeneo matatu ambayo wataalam wa wizara wakiongozwa na Dkt. Kiruswa waliyoweza kuyabaini ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia (high resolution airborne geophysical survey) hususani kwa kuanzia eneo la Mkoa wa Dodoma;

Maeneo mengine ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa fursa kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalam wa ndani katika maeneo ya teknolojia za kisasa kama vile ukusanyaji na uchakataji wa taarifa za jiosayansi; na kusaidia kuleta teknolojia za kisasa za utafiti na uchakataji wa taarifa za utafiti wa madini ikiwa ni pamoja na matumizi ya ndege nyuki katika utafiti wa madini nchini.

# MAONI

## Heko Serikali kwa hili la Kibong'oto

**HIVI karibuni, Waziri wa Afya Jenista Mhagama alisema Hospitali Maalum ya Tiba ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto QA A Taasisi ya Magonjwa A ambayo itakwenda sambamba na uimarishaji wa mifumo ya huduma za tiba ya magonjwa hayo.**

Waziri Mhagama amesema hayo alipofanya ziara katika Hospitali ya Kibong'oto kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo Serikali imetoa fedha ikiwa ni pamoja na eneo la uzalishaji wa gesi tiba na ununuzi wa mashine za kisasa za kuchomea taka.


Alikaririwa akisema, magonjwa ambukizi yanaweza kuibuka mahala popote katika nchi, hivyo kwa uwekezaji mkubwa uliofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan unaiwezesha Tanzania kupambana na magonjwa hayo kwa kuzingatia utaratibu na mifumo ya afya iliyopo.

Aidha, Waziri Mhagama amesema Serikali imewekeza zaidi zaidi ya Shilingi milioni 550 kwa ajili ya kujenga sehemu maalum ya kuchomea taka pamoja na ununuzi wa mashine maalum ya kisasa ambao una uwezo wa kuteketeza taka zaidi ya Kg 400 kwa saa moja katika eneo hilo.

Pia, Waziri Mhagama amesema Serikali kupitia Wizara ya Afya imewekeza zaidi ya Sh bilioni 1.6 kwa ajili ya kutengeneza mradi wa kuzalisha gesi tiba ambao mradi huo umeshakamilika na kuanza kufanya kazi katika hosoitali hiyo, ambao umesaidia kuokoa fedha za kuagiza gesi hiyo kutoka nje.

Kwetu tunapenda kuipongeza Serikali kwa hatua hii, kwani katika dunia ya sasa ambayo ina muingiliano mwingi wa watu kutoka sehemu moja kwenda nyingine ni rahisi pia kupatwa magonjwa ambukizi.

Hivyo kuwa na Taasisi imara ambayo itashughulikia mno magonjwa hayo, ni jambo lililo jema zaidi na linaloleta furaha miongoni mwa Watanzania na kuona Serikali yao inawajali na kuwasikiliza.




# TUFIKIRI PAMOJA

## Mnyororo ongezeko la thamani utapunguza manung'uniko

NA MWIGA MWIGASI

**SERA ya soko huria iliyoanza kutekelezwa toka miaka ya 1990 imefungua fursa kwa wawekezaji kuwekeza kwa wingi kwenye maeneo mbali mbali ya kibiashara.**

Kwa muda mrefu, kilimo kimewavuta wawekezaji ambao wamekuwa wakijishughulisha na mashamba makubwa ili kukudhi madhumuni ya biashara ya kuzalisha kwa wingi kupunguza gharama ya kuzalisha kwa kiasi kidogo.

Pamoja na kutekelezwa kwa makubaliano baina ya wawekezaji na kijiji wanakofanya shughuli za kilimo, kumekuwa na manunguniko mengi kuhusu wawekezaji kuchukua maeneo makubwa na ardhi ikianza kupungua kutokana na kuongezeka kwa watu na wahamiaji hasa wafugaji.

Ili kupungumza manunguniko ya wakulima inabidi wakulima watayarishwe, ili waweze kuzungumza lugha ya biashara ambayo inalingana na ya wawekezaji.

Ni muhimu wakulima wakaelimishwa na kufahamu kwa undani kuhusu kilimo biashara. Hii itawasaidia wakulima kutimiza nia ya kufanya kilimo biashara na kupata kipato kikubwa. Ili kufikia lengo hilo inabidi wakulima wafanye mambo yafuatayo;

Walime kwa kiasi cha kutosha. Wasindike wenyewe na watafute soko na kuuza bidhaa zilizoongezwa thamani badala ya kuuza mali ghafi.

Mkulima anayeuza bidhaa zilizoongezewa thamani anakuwa na fursa ya kushiriki kupanga bei badala ya kupangiwa bei kitendo ambacho kinampa fursa ya kupata faida kubwa.

Wawekezaji wanahamasishwa kuchukua mali ghafi kwa wakulima na kusindika kwa niaba ya wakulima na kuwaunganisha na masoko ya bidhaa wakitumia teknolojia za kisasa ambazo mkulima mdogo hawezi kuzipata kutokana na kuwa na mtaji midogo.

Kuna faida wakulima wadogo kujiunga na wawekezaji wanaofanya shughuli za kilimo kwa kiwango kikubwa. Moja wapo ya faida hizo ni pamoja na mkulima mdogo kuunganishwa na soko ambalo humpatia mkulima midogo faida.

Halikadhalika humuwezesha mkulima mdogo kuongeza uwezo wa kupanua shamba, kupata kipato kikubwa na kupunguza manunguniko. Mkulima ambaye anauza mazao yaliyoongezewa thamani anaweza kupanua kilimo chake na kuongeza idadi ya mazao ambayo anaweza kulima, kusindika na kuongezea thamani.

Vipi kuhusu wafugaji? Wafugaji wanaweza kutumia eneo dogo la ardhi ikiwa wanafuga ndani badala ya kuchunga na kuwa na mkakati wa kutenga maeneo ambayo yataoteshwa malisho kwa ajili ya mifugo.

Kwa kufanya hivyo pia itapunguza migogoro ambayo inatokea kati ya wakulima na wafugaji kwa baadhi ya maeneo kwa sababu ya wafugaji kupenda kuchunga badala ya kufuga ndani.

Kwa kufanya ufugaji wa ndani, itawawezesha pia wafugaji kuuza mifugo iliyoongezwa thamani, kwa mfano kunenepesha mifugo na kuongeza tija ya kupunguza kiasi cha mifugo badala ya kuwa na mifugo mingi isiyokuwa na tija. Mfugaji anaweza kuwa na mifugo michache yenye faida.



# Ukitaka kukopa benki, hizi ndizo njia tano

**TUNAPOZUNGUMZIA ujasiriamali ni lazima kwanza ujue nini maana ya neno hilo ambalo lilianza kutumika miaka ya 1700 likiwa na maana ya kawaida ya kuanzisha biashara.**

Lakini maana ya ujasiriamali kutoka kwa wachumi, ujasiriamali ni kukabiliana na vikwazo za biashara endapo kuna uwezekano wa kupata faida. Kwa wengine ni kuwa na uwezo wa kukwepa vikwazo za biashara ili ufanikishe biashara yenye faida.

Pia wengine wamemuelezea mjasiriamali kama ni mtu mbunifu mwenye uwezo wa kuuza ubunifu wake.

Wachumi wengine wameendelea kumuelezea mjasiriamali kama mtu mwenye kuleta bidhaa au huduma za kibunifu kwenye soko ambazo hazijawahi kuwepo.

Katika karne ya 20, mchumi mmoja kwa jina Joseph Schumpeter (1883-1950) alifafanua kuwa mjasiriamali ni mtu mwenye kuleta ubunifu na maboresho yenye kuleta sio tu hamasa bali pia kuwa kichocheo cha mabadiliko.

Joseph Schumpeter aliendelea kumuelezea mjasiriamali kama "mbunifu mharibifu" maana yake ni kwa kuwepo wajasiriamali na bidhaa au huduma zake, viwanda huduma na au bidhaa dhaifu na za zamani zilikufa na kutoweka kabisa kwenye soko.

Wachumi wengi leo hii wanaamini kuwa mjasiriamali ni moyo na kichocheo katika kukua kwa chumi za nchi mbalimbali duniani.

Lakini maana ya ujasiriamali kutoka kwa wafanyabiashara ilifafanuliwa na Peter Drucker (1909-2005) alielezea wazo hili kwa mapana mengine kuwa, mjasiriamali ni mtu anayepeleleza mabadiliko, kuwa na mwitikio wa haraka na kuhatamia fursa zilizopo katika mabadiliko. Mfano wa hili ni mabadiliko yaliyotokea katika sekta ya mawasiliano kutoka typewriter kwenda kompyuta.

Mjasiriamali anaweza kutokea katika hali yeyote, msomi au sio msomi, mhandisi, mwanasheria au mwalimu mchungaji.

Lakini mjasiriamali huyu anaweza akawa anataka kukopa na akawa anashindwa ajue wapi pa kuanzia, hivyo ni vyema pia ukazijua mbinu tano ambazo unaweza kuzitumia katika kuhakikisha unapata mkopo benki.

Fahamu benki ni mkopeshaji mkubwa na mgumu kwa mazingira ya Tanzania. Pamoja na hayo benki wana masharti maalumu ambayo nayo hutofautiana kulingana na nani anakopa, anakopa kiasi gani na kwa ajili ya biashara ipi na soko lipi.

Kila benki inaweza kuwa na vigezo tofautotofauti. Mikopo mikubwa huambatana na masharti lukuki tofauti na mikopo midogo. Mikopo kwa watu wenye rekodi nzuri ya kulipa ni tofauti na mkopo kwa watu wenye rekodi mbaya au ambao ndio kwanza wanaomba mkopo kwa mara ya kwanza.

Mkopo kwa watu maarufu au makampuni yenye majina ni tofauti kwa watu wasio maarufu au taasisi zisizo na majina.

Ebu tuangalie dondoo hizi hapa chini zitakazokusaidia kujua masharti muhimu ya mabenki:

1.Je ni biashara mpya au inayoendelea?

Biashara inayoendelea na yenye angalau miaka mitatu ina nafasi kubwa kuliko zile changa au mpya

2.Aina ya biashara unayofanya

Biashara za kuzalisha zinanafasi kubwa kuliko zile za huduma au uchuuzi



3. Integrity (historia safi ) ya mkopaji

Historia safi ya mkopaji ya kukopa na kurudisha bila usumbufu inaongeza uwezekano mkubwa wa kupewa mkopo

4. Dhamana na mdhamini wa mkopaji kama akishindwa kurudisha

Kwa bahati mbaya mkopaji akishindwa kurudisha kwa namna yeyote ile mkopo, je kitu gani kitafidia huo mkopo ili benki wasipate hasara au nani atasimama kama mdhamini ili yeye ndie ashikwe endapo mkopaji atashindwa kurudisha mkopo. Aina ya dhamana na mdhamini atakayekubaliwa na benki itasaidia wewe kupata mkopo

5. Mchanganuo wa Biashara

Mchanganuo wa biashara wenye kuonyesha mchanganuo wa kisekta, ushindani, uzalishaji, uongozi/utawala, masoko na mambo ya fedha kwenye fedha hasa mtaji utakaohitajika, makisio ya mauzo, gharama, na faida. pia makisio ya balance sheet na cashflow itatakiwa.

Hii ni pamoja na uwiano wa sehemu muhimu za biashara kama uwiano wa mauzo na matumizi, mauzo na mishahara, mauzo na mtaji, mauzoi na gharama ghafi, muda wa kurudisha gharama na kuanza kupata faida na mengineyo.

# Ramadhani: Mwili wako unapitia katika haya



**KILA mwaka mamilioni ya Waislamu duniani hufunga tangu jua linapochomoza mpaka linapotuwa kwa siku 30 mfulilizo katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.**

Katika miaka ya hivi karibuni, Ramadhan hujiri katika miezi ya joto na katika maeneo ya kaskazini hilo mara nyingine humaanisha watu kufunga kwa saa nyingi na katika hali ya hewa yenye joto jingi.

Baadhi ya nchi kama Norway, waumini hufunga kwa hadi saa 20 kwa siku mwaka huu. Basi hili lina manufaa yoyote? Haya ndiyo yanayofanyika mwilini mwako unapofunga kwa siku 30.

**Siku za kwanza**

Kimsingi mwili wako hauingii katika hali ya kufunga mpaka saa nane au zaidi baada ya kula chakula chako cha mwisho. Huu ndio wakati utumbo unamaliza kusaga chakula na kunfyonza madini kutoka chakula ulichokila.

Muda mfupi baada ya hili, mwili wetu huanza kutafuta glucose iliopo kwenye maini na misuli kutafuta nguvu mwilini.

Muda unavyosogea, baada ya glucose iliopo mwilini kumalizika, miwli hugeukia mafuta kutafuta nguvu.

Mwili unapoanza kuchoma mafuta, hili husaidia kupunguza uzito wa mwili, hupunguza viwango vya cholesterol na kupunguza hatari ya kuugua kisukari.

Hata hivyo kushuka kwa vinwango vya sukari mwilini inasababisha mwili kudhoofika na kukosa nguvu. Huenda ukaanza kuumwana kichwa, ukasikia kisunzi, kichefuchefu na harufu mbaya kutoka mdomoni.

**Kiwango cha njaa**

Jihadhari na mwili kupungua maji- Siku ya 3-7

Mwili unapoanza kuzoea kufunga, mafuta yanayayuka na kugeuka sukari mwilini.

Ni lazima ujirudishie maji mwilini kufidia masaa uliokuwa umefunga, la sivyo unapotokwa na jasho unaweza kupungua maji mwilini.

Ni muhimu chakula chako kijukuisha 'lishe yenye kukupa nguvu', kama vile vyakula vyenye uwanga na vya mafuta kidogo. Ni muhimu kuwa na lishe bora, ikiwemo protini, chumvi na maji.

**Siku ya 8-15**

Katika awamu ya tatu, utaona hali inaimarika, kama vile hisia wakati mwili unaanza kuzoea kufunga.

Dkt. Razeen Mahroof, mshauri katika Hospitali ya Addenbrooke huko Cambridge, Uingereza anasema kuna manufaa mengine.

"Katika maisha yetu ya kawaida huwa tunakula vyakula vyenye kalori nyingi tu,na hili huweza kuuzuia mwili kutekeleza majukumu mengine kama kujirudisha katika hali yake ya kawaida.

"Hili husawazishwa wakatimtu anapofunga, huruhusu mwili kuangazia kazi nyingine. Kwa hivyo kufunga huenda kukaunufaisha mwili kwa kuuponya na pia kuzuia na kupambana na maambukizi."

**Siku ya 16 -30**

Katika nusu ya mwisho ya Ramadhan, mwili wako utakuwa umeshazoea kabisa kufunga. Maini, figo na utumbo na ngozi yake zitakuwa zinajitakasa kufikia sasa.

"Kiafya, kufikia kiwango hichi viungo vyako ndani ya mwili vimerudi kufanya kazi kikamilifu , huenda kumbukumbu yako ikawa imeimarika na ukawa na nguvu zaidi," anasema Dkt Mahroof.

"Mwili wako hautafuti protini ya kuupa nguvu hili ni wakati uanapokuwa na 'njaa' na kutumia misuli kuupa nguvu. Hili hufanyika iwapo utafunga kwa muda mrefu mtawalia.

"Kwasbabau watu hufunga ramadhan tangu alfajiri mpaka jioni, kuna nafasi nzuri ya kurudisha nguvumwilini kutokana na vyakula na vinywaji. Hii huhifadhi misuli lakini pia husaidia katika kupunguza uzito mwilini."

**Kufunga kuna manufaa?**

Dkt. Mahroof anajibu ndio, lakini kwa sharti moja. "Kufunga kuna manufaa kwa afya yetu kwasababu inatusaidia kulenga tunachokula na wakati tunapokila. Hatahivyo japo kufunga kwa kipindi cha mwezi mmoja ikawa ni sawa, sio vizuri kufunga mfululizo baada ya Ramadhan.

'Kufunga mfululizo sio vizuri katika kutafuta kupunguza uzito wa mwili kwasbabau hatimaye mwili utaacha kugeuza mafuta kuwa nguvu na badala yake utageukia misuli. Hili sio jambo zuri na ina maana mwili wako utaishia kudhoofika kwa njaa.'

Anapendekeza kwamba kufunga kando na katika mwezi wa Ramadhani au kufunga kwa siku tano na kupumzika siku mbili ni vizuri kuliko kuamua kufunga kwa miezi kadhaa mfululizo.

"Ukifunga mwezi wa Ramadhan vizuri, itakuruhusu kuirudisha nguvu mwilini, jambo linalomaanisha kwamba huenda ukapunguza kilo mwilini bila ya kupoteza misuli yako."



# Maharagwe machanga; Fedha ardhini

**HIVI karibuni hapa nchini, kumekuwa na uanzishaji na uendelezaji wa kilimo cha mazao mapya ambayo hayakuzoeleka hapo awali. Moja ya mazao hayo ni pamoja na maharagwe machanga, maarufu kama 'Green beans' au 'French beans'.**



Mbegu inapendekezwa kutumia chotara aina ya F1. Aina hii ya mbegu imeonekana kuwa na mafanikio makubwa zaidi ikiwa ni pamoja na uwezo wa kumudu magonjwa. Inapendekezwa kupata mbegu kutoka kwa wazalishaji walioidhinishwa.

**Aina za mbegu na uwezo wake**

Boston: Aina hii ya mbegu ina uwezo mkubwa wa uzalishaji. Wakati wa mvua aina hii ya mbegu hushambuliwa zaidi na magonjwa hasa ya ukungu.

Serengeti: Aina hii ina uzalishaji wa wastani. Aina hii ina uwezo mkubwa wa kuvumilia magonjwa.

Tana: Aina hii uzalishaji wake ni mkubwa na wa muda mrefu. Inashambuliwa na magonjwa kwa wastani. Aina hii huhitaji kiwango kikubwa cha maji hasa wakati wa mavuno.

Maharagwe machanga yamegawanyika katika makundi mawili;

Maharagwe mateke kwa wastani (fine beans)

Maharagwe mateke zaidi (extra fine **beans)**

**Utayarishaji wa shamba**

Lima shamba na kuondoa magugu yote. Hakikisha kuwa umelima kwa kiwango ambacho udongo umelainika vya kutosha. Kabla ya kupanda ni lazima uhakikishe udongo umelainika vizuri na una maji ya kutosha siku mbili kabla ya kupanda. Hii inategemeana na aina ya umwagiliaji, kwenye kilimo cha maharagwe machanga inapendekezwa zaidi kutumia umwagiliaji wa matone.

**Kupanda**

Inashauriwa kuweka nafasi ya sentimita 30 kati ya mstari na mstari, na kati ya mmea na mmea sentimita 7. Panda mbegu moja kwa kila shimo. Panda kwenye tuta na liwe na upana wa sentimita 70, kati ya tuta na tuta kuwepo nafasi ya sentimita 80.

Ni vizuri kuacha nafasi ya sentimita 15 kutoka pembeni mwa tuta unapopanda mbegu, ili kuepusha athari zinazoweza kutokea na kuathiri mbegu au mmea baada ya kuota, mfano, mafuriko.

Endapo unatumia umwagiliaji wa mifereji inashauriwa kutengeneza makingo yenye kimo cha sentimita 15 na upana wa sentimita 70 kutoka kingo hadi kingo. Hii itasadia mimea kupata unyevu kwa urahisi pamoja na kinga ya magonjwa yanayosababishwa na unyevu uliopitiliza.

Mbolea

Inashauriwa kutumia mbolea hai iliyoiva vizuri kiasi cha … kwa ekari moja. Pia, unaweza kupandia zinazotokana na miamba kama vile DAP. Tumia gramu 5 kwa kila shimo. Hii itasaidia mizizi kuota kwa haraka. Usifukie mbegu kwa zaidi ya inchi 1.5. Mbegu za maharagwe machanga huota baada ya siku saba. Endapo mbegu hazikuota vizuri unaweza kurudishia si zaidi ya siku mbili tangu maharagwe yote.

Umwagiliaji

Hii inategemeana na hali ya hewa/msimu, kulingana na eneo ulipo. Kwa kawaida maharagwe haya hustawi kwenye udongo usiotuamisha maji, na iwe kwenye ukanda wenye baridi ya wastani.

**Utunzaji**

Inapendekezwa kuwasiliana na mtaalamu wa kilimo alie karibu nawe baada ya siku 14 ili kufanya ukaguzi shambani kuona kama kuna dalili zozote za wadudu pamoja na magonjwa kama vile mnyauko fuzari, endapo kuna dalili zozote shauriana na mtaalamu.

Mkulima anaweza kutumia mbolea kwa ajili ya kukuzia na kurutubisha majani kulingana na mahitaji. Ni lazima kupanda mahindi kuzunguka shamba la maharagwe ili kuzuia upepo unaoweza kuharibu maharagwe yako na yasiwe na ubora unaotakiwa.

**Palizi**

Ni muhimu kufanya palizi kuanzia baada ya siku kumi ili kuepusha makazi/maficho ya wadudu waharibifu. Unaweza kunyunyiza dawa ya kuzuia kutu baada ya wiki tatu.

Maharagwe machanga huchukua wiki 9-10 tangu kupanda hadi kuvuna. Hii inategemeana na hali ya hewa pamoja na mbegu. Maharagwe haya huchanua baada ya wiki sita. Wakati huu mkulima anatakiwa kuwa makini sana kutokana na uwezekano wa kuwepo wadudu waharibifu kama vile thiripi.

Inapendekezwa kuwasiliana kwa karibu na mtaalamu wa kilimo ili kufanya ukaguzi ili kubaini aina ya wadudu na hatua za kuchukua.

**Uvunaji**

Maharagwe machanga yanafaa kuvunwa viriba vinapokuwa na urefu wa sentimita 11.5 15, unene wa milimita 6-8. Hii hufanyika katika wiki ya 9-10. Ili kupata soko zuri, pata maelekezo ya namna ya kuvuna kutoka kwa wataalamu walio karibu nawe.

# DONALD TRUMP AIGEUKA UKRAINE



**RAIS wa Marekani Donald Trump amesitisha misaada yote ya kijeshi kwa Ukraine kufuatia mzozo wake na Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy wiki iliyopita, amesema afisa wa Ikulu ya White House.**

"Rais Trump amekuwa wazi kuwa anataka amani. Tunataka pia washirika wetu wajitolee kwa lengo hilo. Tunasitisha misaada yetu na kuikagua ili kuhakikisha inachangia katika suluhu," alisema afisa huyo, akizungumza kwa sharti la kutotajwa jina.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, Ikulu ya White House haijaeleza aina na kiasi cha misaada itakayositishwa au muda wa kusitisha utadumu kwa kipindi gani. Pentagon pia haijatoa maelezo zaidi.

Ofisi ya Zelenskiy haijatoa majibu kwa maswali ya Reuters kupitia Ubalozi wa Ukraine huko Washington.

Hatua hiyo imekuja baada ya Trump kupindua sera za Marekani kuhusu Ukraine na Urusi alipoingia madarakani mwezi Januari, na kuchukua msimamo wa urafiki zaidi kwa Moscow.

Haya yanakuja baada ya mabishano makali kati ya Trump na Zelenskiy katika Ikulu ya White House siku ya Ijumaa ambapo Trump alimtuhumu kwa kutoshukuru vya kutosha kwa uungaji mkono wa Washington katika vita na Urusi.

Mara baada ya Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky kufukuzwa Ikulu ya Marekani kufuatia malumbano yake na Rais Donald Trump na Makamu wa Rais JD Vance, viongozi wa Ulaya walituma jumbe nyingi kumuhakikishia kwamba watasimama naye hadi dakika ya mwisho

Siku iliyofuata tu ya Jumamosi iliyopita, Zelensky alitua Uingereza, akaonana na Waziri Mkuu wa nchi hiyo Kier Starmer na hata kufanya mazungumzo na Mfalme Charles. Siku ya Jumapili akakutana na viongozi wengine wa Ulaya waliokutana London kujadili mustakabali wa usalama wa bara lao

Pamoja na maonyesho yote haya, swali kubwa ni; Ulaya ina ubavu wa kuisaidia Ukraine kijeshi ikiwa Marekani itakaa pembeni?

Jibu la haraka ni; Hapana, haina uwezo huo katika uvamizi huu wa sasa wa Urusi

## Uhaba wa bajeti

Kuna vitu vingi Ulaya inahitaji kuweka sawa, muda ni mchache na haina utashi wa kisiasa wa kutosha

Ukianza na bajeti ya kijeshi tu, kwa mujibu wa International Institute of Strategic Studies, bajeti ya kijeshi ya Urusi kama nchi ni kubwa kuliko ile ya bara zima la Ulaya. Wakati Urusi imetenga 6.7% ya pato lake la taifa, wakati Ulaya (wanachama wa Nato ukiondoa Marekani) wanatumia wastani wa 1.6%.

Ili kukabiliana na Urusi, wataalamu wanasema Ulaya itapaswa kuongeza matumizi yake ya kijeshi hadi kufikia wastani wa 3.5% ya pato la taifa la umoja huo, hasa kwa nchi za Mashariki ya Ulaya zilizo karibu na Urusi kama vile.

Tayari tunaona nchi kadhaa za Ulaya zimeanza kuongeza bajeti yao ya kijeshi. Uingereza kwa mfano, siku chache zilizopita imetangaza mpango wa kukata pesa inayotuma kwa misaada nje ya nchi na kuielekeza katika bajeti yake ya ulinzi.

## Uwanja wa mapambano

Kuhusu wanajeshi walio tayari kupigana, wakati Urusi ina wanajeshi takribani 250,000 walio tayari kupelekwa Ukraine muda wowote, Ulaya haiwezi kutoa wanajeshi 150,000, ambao Zelensky anasema watahitajika kulinda amani na kumzuia Putin asivamie tena.

Viongozi wengi wa Ulaya wamesema wakijitahidi sana, basi wanaweza kupeleka wanajeshi wasiozidi elfu thelathini (30,000).

Ulaya inakabiliwa na ukosefu wa kiongozi mmoja (mtu au ofisi) wa kijeshi. Kwa ujumla Ulaya (wanachama wa Nato) ina wanajeshi wapatao 1.47 ambao wako tayari kupigana, lakini hawana komandi moja ya kuwakusanya na kuwaongoza. Kwasasa Nato inategemea hii kazi kufanywa na Marekani.

Hivyo Marekani akikaa pembeni, Ulaya itakuwa na kazi ya kutafuta kiongozi ambaye anaweza kuvikusanya, kuvijumuisha na kuviongoza vikosi vya nchi zote za Ulaya wanachama wa Nato kuwa kikosi kimoja chenye nguvu, badala ya kila nchi kwenda kukabiliana na Urusi kama nchi moja moja.

Ulaya ina teknolojia ya kutosha, lakini inahitaji uwekezaji mkubwa kuanza kutengeneza vifaa vikubwa na bora zaidi hasa vya masafa marefu kama ambavyo Marekani imetoa kwa Ukraine ndani ya miaka hii mitatu

Silaha za anga na utashi wa kisiasa

Nchi za Ulaya pia zinategemea vifaa vya anga vya Marekani na uwezo wake mkubwa wa kukusanya intelijensia, uwezo ambao Ulaya haina.

Hata katika usafirishaji wa silaha, Ulaya imekuwa ikitegemea sana miundombinu na uratibu wa Marekani kufanikisha kusafirisha msaada wa vifaa uliopeleka Ukraine.

Wakati Nato inavamia Libya mwaka 2011, hata kama Ulaya ndio ilikuwa inaongoza mapambapo, walitegema zaidi vituo vya mafuta vya Marekani kujaza vifaa vyao.

Ulaya inahitaji kiongozi katika masuala ya dunia, kama ambavyo Marekani imekuwa. Aidha Ujerumani au Ufaransa inaweza kuchukua nafasi hii, lakini nchi tatu; Ujerumani, Ufaransa na Uingereza zinahitaji kuwa katika ukurasa mmoja, zikazungumza lugha moja na zikawa na utayari wa pamoja kuongoza nchi zingine 27 za Nato katika kuikabili Urusi.

Mbali na uwezo wa kifedha na kijeshi, nchi nyingi za Ulaya zinakabiliwa na mikingamo na mivutano ya kisiasa ndani ya nchi zao, zingine zikiwa na idadi kubwa ya wananchi wasiotaka nchi zao kujihusisha moja kwa moja na vita kwa ujumla na hasa mapigano na nchi kubwa kama Urusi.

Utayari wa serikali nyingi za Ulaya kuingia vitani na Urusi kutategemea utashi wa kisiasa na wananchi kwa ujumla kutoka nchini mwao, jambo ambalo ni changamoto kwa nchi nyingi za Ulaya.

# Unafuga kondoo? Zalisha chotara

**NJIA ya haraka zaidi ya kuboresha kundi lako ni kuzalisha kondoo chotara. Inashauriwa utumie kondoo wa kienyeji kama wanyama wa kuanzia mpango wa kuzalisha kondo bora zaidi.**

Unaweza kutumia kondoo jike wa kienyeji aina ya Red Maasai na dume wa kigeni aina ya Dorper. Kondoo wanaozaliwa watabeba sifa za aina hizi mbili za kondoo (Red Maasai na Dorper).

Njia hii ya kuboresha kondoo ni ya gharama ya chini ikilinganishwa na kununua wanyama waliokwisha kuboreshwa, ambao mara nyingi huuzwa kwa bei ya juu.

**Mpango wa uzalishaji**

Weka mpango mzuri wa ufugaji ambao ni pamoja na kumbukumbu za wanyama zilizohifadhiwa vizuri ili kuzuia kuzaliana kondoo wenye uhusiano wa karibu.

Kondoo wa kienyeji wanaweza kuboreshwa zaidi kwa muda mfupi ikiwa kuna mipango thabiti, usimamizi bora na uzalishaji wa hali ya juu. Chagua kondoo jike walio na maumbile mazuri, mwili mrefu na mifupa yenye nguvu.

Kwa njia hii unapata kondoo wenye mwili mkubwa na nyama nyingi. Tumia kondoo jike na dume wenye ubora wa hali ya juu kuzalisha. Usitumie kondoo wafupi na wenye mwili mdogo. Vigezo vingine vya uteuzi ni pamoja na ukuaji wa haraka, afya njema na uwezo wa kuzaa mapacha.

Uza Kondoo wasio na ubora na tumia pesa kununua kondoo jike wengine ili uweze kuongeza idadi ya kondoo haraka. Pia, tumia pesa kununua dawa za kudhibiti magonjwa na wadudu.

**Ufugaji ulioboreshwa**

Kuboresha kondoo kwa kuzalisha chotara huenda sambamba na ufugaji ulioboreshwa; lishe, makazi, na udhibiti wa magonjwa.

Bila usimamizi bora, kondoo walioboreshwa wanaweza wasifanye vizuri; wanaweza kufanya vibaya zaidi kuliko wale wa kienyeji, kinyume na matarajio ya mfugaji.

Wanyama waliolishwa vibaya hawahimili magonjwa na vimelea. Hawaingii kwenye joto haraka, uzalishaji wao wa maziwa ni duni na wana-kondoo wao ni dhaifu na hukua taratibu.

Mabanda safi, maji safi, malisho bora na virutubisho vya madini ni muhimu. Kondoo wanakula nyasi iliyo karibu na ardhi tofauti na ng'ombe na mbuzi.

Mbuzi wanapendelea vichaka. Hivyo basi, kuwa makini na idadi ya kondoo kwenye malisho. Ikiwezekana, zungushia maeneo ya malisho ili kutoa nafasi kwa malisho muda wa kupoa na kukua tena. Unaweza kuwalisha kondoo nyasi iliohifadhiwa wakati wa jioni wanapopumzika.

**Tumia dume wa Dorper**

Kondoo wa Dorper ni mseto kati ya kondoo wa Blackhead Persian (uzao wa Kiafrika) na Dorset Horn (uzao wa Uingereza), uliozalishwa Afrika Kusini.

Ni kondoo mwenye mafanikio makubwa na ameuzwa kwa nchi nyingi. Kuna aina mbili: 'Dorper' mwenye kichwa cheusi, na 'White Dorper' mwenye kichwa cheupe. Wafugaji wengi wamemzoea 'Dorper' mwenye kichwa cheusi.

Kondoo wa Dorper hufanya vizuri katika maeneo mengi kutoka nyanda za juu hadi maeneo yenye ukame. Wana uwezo mkubwa wa kuzaliana na wanaweza kuzaa kila baada ya miezi 8. Wana-kondoo huongeza uzito haraka, hukomaa mapema na huweza kupandishwa ndani ya miezi 9.

Kondoo wa kienyeji (kama kondoo wa Kimasai) hupandishwa kondoo dume wa Dorper. Kondoo wa kike wanaozaliwa pia wanapandishwa tena dume wa Dorper wasiohusiana.

Kwa kufanya hivi, unachanganya sifa nzuri za kondoo wa kienyeji na kondoo wa kigeni. Unazalisha angalau mara mbili ili kupata kizazi kizuri chotara.

**Zuia kuzaliana ndani**

Kondoo dume hapaswi kupandishwa kwa dada zake, binti, wajukuu, mama au bibi/nyanya. Weka rekodi na utumie mfumo ambao unaruhusu kutambua kila mnyama na wazazi wake, angalau mama na baba, bibi na babu.

Kondoo dume hapaswi kutumika katika kundi moja ya kondoo jike zaidi ya mwaka mmoja. Kondoo dume wanapaswa kuzungushwa mara kwa mara kati ya watumiaji na vikundi vya wakulima.



Picha: IN Kondoo aina ya red masai



# Mbinu za asili bora kilimo ikolojia

**ILI kutekeleza utunzaji asilia wa mazao ni muhimu sana kuelewa mbinu asilia za kufanikisha kilimo. Kwa hali hiyo matukio na majanga ya kushambuliwa na wadudu waharibifu yanaweza kupunguzwa na utumiaji wa hatua za utunzaji wa mazao.**



Miongoni mwa mbini zinazoweza kutumika katika utunzaji wa mazao kwa njia za asili ni pamoja na;

Kuelewa mfumo wa uhusiano wa viumbe na mazingira ya kilimo

Aina za wadudu waharibifu na wadudu na wadudu wenye manufaa katika shamba lililolimwa na katika eneo la jirani.

Bayolojia ya wadudu waharibifu, magonjwa na wadudu wenye manufaa. Hii ni pamoja na maumbile, mzunguko wa maisha, tabia ya kuzaliana, tabia za kula, na mengineyo.

Utaratibu unaojirudia wa wadudu, katika misimu mbalimbali na kutegemea kwao hali ya mazingira.

Aina ya madhara wakati wa mzunguko wa maisha ya wadudu yatakayosaidia katika mbinu zaidi za kuwadhibiti vizuri.

Msimu au hatua ya ukuaji wa mmea shambani ambapo ni hatari zaidi kushambuliwa na wadudu.

Mimea mingine inayolimwa au mingine ya porini, inayowavutia wadudu maalumu waharibifu.

Wadudu marafiki au vimelea wanaoweza kutumiwa kuwala wadudu hao waharibifu.

**Kilimo mchanganyiko**

Mazao ya aina mbalimbali yanayolimwa sambamba na maua au mimea ya porini yatasababisha yatasababisha mfumo wa aina tofauti utakaosaidia kuwepo kwa maskani na chakula kwa aina mbalimbali za ndege, wadudu na wanyama watambaao(Jamii ya mijusi), ambao pia hupunguza aina Fulani ya wadudu waharibifu wa mazao.

**Hali ya ardhi**

Maeneo yasiyolimwa kama vile miteremko mikali ya milima, maeneo yasiyofikika au yaliyozungushiwa mimea ni maskani mazuri kwa ndege, wadudu na wanyama watambaao (jamii ya mijusi) wanaowinda wadudu waharibifu.

Kubadilisha na kuchanganya mazao

Madhumuni makubwa ya kubadili mazao ni kutenganisha aina fulaniya wadudu waharibifu wa mazao fulani, ambao kukosekana kwa zao hilo huwafanya wahame au kufa kwa kipindi hicho.

Ni vizuri kubadilisha mazao ambayo si ya jamii moja. Katika msimu unaofuata, yaani mazao yanayoshambuliwa zaidi na wadudu fulani, sharti yabadilishwe na yale ambayo mdudu huyo hayapendelei.

Kwa mfano, ili kuzuia bungu wa mahindi, ni vizuri baada ya kuvuna mahindi msimu unaofuata maharagwe yaoteshwe. Hali hii huharibu mzunguko wa maisha ya bungua wa mahindi. Ni vizuri pia kuchanganya mazao ili kupunguza mashambulizi ya wadudu.

Matukio asilia yanayojirudia na wakati muafaka wa kupanda

Kuchagua wakati muafaka wa kupanda kunaweza kupunguza mashambulizi.

Kufahamu mzunguko wa maisha ya wadudu na mahusiano yake katika mazao yanayoshambuliwa humrahisishia mkulima kuchagua muda wa kupanda. Kutokana na hili, mkulima anaweza kupanda mapema au kuchelewa kupanda, ili kuepuka kipindi ambacho wadudu huzaliana kwa wingi.

Kwa mfano; Nyanya zilizopandwa wakati wa kiangazi, hazipati magonjwa ya ukungu kwani hakuna maji ya kuzidi kiasi yanayolowanisha majani ili kuwezesha vimelea vya ukungu kuota.

Mfano; Msimu wa kwanza wa kilimo: Mboga za majani kama mchicha, chainizi, kabichi n.k Msimu wa pili wa kilimo: Mboga za matunda kama nyanya, bamia, bilinganya. Msimu wa tatu wa kilimo: Mazao ya mizizi kama viazi vitamu, viazi mviringo, mihogo. Msimu wa nne wa mazao: Jamii ya mikunde, maharagwe, kunde, mbaazi.

Mbolea na afya ya mimea

Mimea yenye afya nzuri zaidi hustahimili athari iletwayo na magonjwa na wadudu waharibifu na kutoa mavuno mengi. Mbolea huwa na wadudu marafiki ambao hurutubisha ardhi.

Ulimaji ardhi

Utifuaji wa ardhi kwa jembe la kukokotwa na ng'ombe au trekta una lengo la kuuairisha funza na hatua nyingine ya kukua kwa wadudu waharibifu waliobaki ardhini au kwenye mabua ya mazao.

Kwa kuwachimbua wataunguzwa na jua na kuliwa na wanyama na ndege. Mabaki ya mazao hufukiwa na hivyo kukutana na viumbe wa ardhini au unyevunyevu ambao huyaozesha na kurutubisha ardhi.

Uteuzi wa aina bora ya mbegu

Uteuzi wa aina ya mbegu inayostahimili wadudu au magonjwa, husababisha wadudu waharibifu na magonjwa kushindwa kuzaliana.

**Usafi wa shamba**

Usafi wa shamba husaidia kuharibu mzunguko wa maisha ya wadudu waharibifu, wadudu waharibifu kukosa maskani.

**Kupanda kwa nafasi**

Kupunguza kivuli, kupunguza matawi, kuondoa maotea na kushikilia mimea kwa miti ili isilale ardhini. Matendo yote haya husababisha mazingira yasiwe mazuri kwa maendeleo ya vimelea vya magonjwa na wale wadudu waharibifu wapendao kuishi kwenye hali ya kivuli.

Masuala ya kijamii Utunzaji wa mimea ni jukumu la jamii nzima

Mkulima binafsi hawezi kamwe kuchukua hatua zinazofaa kupambana na wadudu waharibifu wanaoenea sehemu kubwa mwenyewe. Hapa ni mahali pazuri pa kufikiria kushirikiana na majirani, ili kuchukua hatua ya pamoja kukabilina na janga la wadudu.

Iwapo hatua za kudhibiti wadudu zitatumiwa baadhi ya mambo ya msingi hayana budi kuzingatiwa:

Kuondolewa au kukomeshwa kabisa kwa wadudu waharibifu wa mazao si jambo zuri. Matokeo au athari zake zisizo dhahiri katika mahusiano ya chakula ni mabaya kwa ujumla na hayawezi kamwe kufidiwa na wingi wa mavuno.

# Usiudharau mchicha, ulime sana



**WAKATI wakulima wakijikita kwa kiasi kikubwa kwenye mazao mengi ya bustani kama vile nyanya, karoti, kabichi na mengine mengi, hawana budi pia kuweka mkazo katika zao la mchichi ambalo huvunwa kwa muda mfupi (wiki 3 – 5) na lenye pato kubwa katika masoko makubwa.**

Pia, mkulima hawezi kuwa na gharama kubwa kwenye kilimo cha mchicha hasa kwa kuwa ni zao la muda mfupi, hivyo suala la wadudu na magonjwa siyo tatizo kubwa.

**Aina za mchicha**

Mchicha upo wa aina mbalimbali na huweza kutofautishwa kutokana na majani, umbo lake pamoja na rangi ya majani.

Aina ya kwanza ni zile zenye majani makubwa ya kijani na yenye kimo cha mita 2 hadi 2.5 na ambayo huzaa majani mengi na yenye ladha ya utamu.

Aina ya pili ni zile zenye majani ya ukubwa wa kati, kimo kifupi cha mita 1.5 na yenye kuzaa majani mengi sana.

Aina nyingine ya mchicha ni ile yenye miiba na mashina, yenye majani na maua ya rangi ya zambarau au nyekundu.

**Kusia**

Mkulima anunue aina ya mbegu anayohitaji kupanda na kusia kulingana na aina ya mavuno anayopendelea kwa ajili ya soko.

Usiaji/upandaji wa kutawanya kwa uvunaji wa kung'oa

Njia hii ya kusia mchicha ni rahisi na ya haraka sana. Mkulima atahitajika kuandaa shamba lake vizuri kwa kuchanganya udongo na samadi au mboji kiasi cha kilogramu 2 kwa mita moja ya mraba.

Kwa majira ya kiangazi wakati ambapo kuna uhaba wa maji, mkulima aandae matuta yaliyo chini ya ardhi (sunken) au bapa na matuta yaliyoinuka toka kwenye usawa wa ardhi kwa wakati wa mvua.

Mkulima achukue mbegu za mchicha na kuchanganya na mchanga kwa (mbegu ni ndogo sana) katika uwiano wa moja kwa tatu (1: mbegu na 3: mchanga) ili kurahisisha usiaji na uotaji ulio katika mpangilio mzuri.

Baada ya hapo, mbegu hiyo ifukiwe kwa tabaka la udongo kwa sentimeta 0.5 hadi 1.0 kisha kunyunyiziwa maji kiasi kidogo ili kuweka unyevu.

**Palizi**

Miche inapoota, mkulima afanye palizi walau mara 1 kwa juma ili kuondoa ushindani wa magugu na mchicha pamoja na kuepuka mchanganyiko wa magugu wakati wa kuvuna.

Aidha, mimea ipunguzwe kwa umbali wa sentimeta 5 toka mmea na mmea ili kupata mimea bora, imara na yenye afya. Katika upandaji huu, mkulima huweza kuvuna mchicha baada ya wiki 3 toka kusia hadi 5 ikiwa ni kwa kutegemea aina ya mchicha uliosiwa.

Usiaji wa muda mrefu katika mistari kwa uvunaji wa kuchuma

Mkulima achague mbegu anayohitaji kupanda na kuandaa vitalu kisha kuchanganya mbegu na mchanga na kusia kwa umbali wa sentimeta 20 hadi 30 kutoka mstari na mstari. Shamba liandaliwe kwa kulimwa vizuri na kuchanganywa udongo na samadi au mboji iliyoiva kwa uwiano wa kilogramu 2 hadi 5 kwa mita moja ya mraba.

Baada ya majuma 3, miche ing'olewe na kuhamishiwa kwenye shamba lililoandaliwa na kuoteshwa kwa nafasi ya sentimeta 10 hadi 15 kutoka mmea hadi mmea.

Palizi

Usafi wa shamba yaani palizi ifanyike kila wiki mara 1 ili kuondoa magugu yanayotafuta virutubisho kwa ushindani pamoja na mchicha.

**Uvunaji**

Mchicha uvunwe baada ya wiki ya 5 hadi 7 toka kupandwa na kuendelea hadi miezi 4. Mimea ya zamani inaweza kukatwa karibu na usawa wa ardhi na kuchipua.

Wadudu na magonjwa

Zao la mchicha haliathiriwi sana na magonjwa wala wadudu kama mazao mengine ya bustani. Wadudu kama vidukari na utitiri huweza kuathiri zao hili hasa zile zilizozeeka na kwa baadhi ya aina ya mchicha huweza kuathiriwa na virusi.

**Masoko**

Uvunaji wa ung'oaji mmea mzima na uuzaji unafanyika kwenye masoko ya kawaida kwenye miji mikubwa na midogo. Aidha, bei ya uuzaji wa mafungu ya mchicha hapa Tanzania huwa ni shilingi 100 hadi 200 lakini bei huwa juu kwenye masoko makubwa.

**Uzalishaji wa mbegu**

Kwa uzalishaji wa mbegu za aina zote za mchicha, inashauriwa kupanda kwa nafasi ya sentimeta 60 toka mstari hadi mstari na sentimeta 25 tika mche na mche.

Mbegu zikishakoomaa huvunwa na kukaushwa kisha kupigapiga ili kutoa mbegu.



# Fuga samaki, changanya na mazao mengine

**KATIKA Makala haya tutatazama kwa kina zaidi juu ya ufugaji mseto wa samaki na mazao mengine, ikiwa pamoja na kutazama faida za ufugaji huo, pamoja na manufaa ya ufugaji wa namna hiyo.**

Aina ya samaki wanaofaa katika kilimo mseto ni Perege na Kambale, ambao ni samaki wanaofugwa katika maeneo mabalimbali nchini Tanzania. Perege ndiyo aina ya samaki inayofahamika zaidi kwa wafugaji.

Chakula cha asili cha Perege ni vimelea vya kijani vilivyomo ndani ya maji, lakini ana uwezo wa kula aina nyingi za vyakula ikiwa ni pamoja na pumba za mahindi na mpunga, majani na mabaki ya jikoni.

Vile vile anakua vizuri kama kutakuwa na mbolea za samadi na za chumvi chumvi, na anaweza kuhimili kiasi kidogo cha hewa ya oksijeni.

Madume ya Perege hukua haraka zaidi kuliko majike, na uvunaji unaweza kufanyika baada ya kufikisha uzito wa gramu 250. Kambale hula vyakula vya asili ndani ya maji kama vile wadudu, konokono, vifaranga wa chura na samaki wengine wadogo.

Vile vile anakula vyakula vya ziada kama vile mabaki ya vyakula hasa yenye asili ya nyama. Kambale hutumika kupunguza wingi wa Perege ndani ya bwawa.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba Perege anazaliana kwa wingi kwenye bwawa. Kambale anakua haraka sana kama chakula chenye protini kinapatikana kwa wingi.

Kambale anaweza kuishi kwenye maji yenye hewa kidogo ya oksijeni. Tofauti na Perege, Kambale ana mifupa michache na minofu mingi na ni mtamu hasa anapokaushwa kwa moshi.

**Faida za mboga mboga katika ufugaji mseto**

Chanzo cha chakula cha samaki: Mboga mboga hutumika moja kwa moja kama chakula cha samaki kwa kuwa jamii ya samaki wengi wanaofugwa ni wale wanao kula majani kama jamii ya Sato na Perege na hata jamii ya Kambale.

Hivyo mabaki ya mboga mboga kutoka bustani hukatwa katwa vipande vidogo vidogo kwa ajili ya kulisha samaki.

Chakula cha mkulima: Hili huwa lengo kuu la kulima mboga mboga kwenye mseto na ufugaji samaki. Chakula jamii ya mimea huwa na kiwango kikubwa cha madini yanayohitajika katika utunzaji wa afya ya mwanadamu.

Mboga mboga hupunguza gharama ya ununuzi wa chakula kwa mkulima kwa kumwezesha mkulima kupata lishe bora kutoka shambani kwake.

Chanzo cha fedha: Ufugaji mseto wa samaki na bustani hulenga kuwa kitega uchumi kikubwa kwa wakulima wadogo.

Mavuno ya mazao ya bustani huuzwa kirahisi kwa kuwa yanahitajika kwa wingi na jamii kutokana na umuhimu wake.

Fedha inayopatikana husaidia katika utunzaji wa shamba mseto au kutumika katika mahitaji mengine ndani ya familia ya mfugaji.

Mbolea kwenye bwawa la samaki: Mboga mboga hutumika kama mbolea kwenye bwawa la samaki. Mboga mboga huozeshwa kwenye hori ili iwe mboji ambayo hutoa mimea na wadudu wa asili ambao hutumika kama chakula cha samaki. Hii hupunguza gharama za uzalishaji kwenye bwawa la samaki.

**Faida za kuku katika ufugaji mseto**

Chanzo cha mbolea: Lengo kuu la ufugaji wa kuku kwenye ufugaji mseto ni urutubishaji wa bwawa la samaki ili kupata chakula cha asili kwa samaki. Kinyesi cha kuku hutumika kama chanzo cha mbolea kwa sababu kina kiasi kikubwa cha urea.

Hutoa chakula cha samaki: Tofauti na kuwa chanzo cha rutuba, kinyesi cha kuku huliwa moja kwa moja na samaki.

Hiki huwapa samaki afya nzuri kwani huwa na chembechembe nyingi za urea, ambazo ni sehemu kubwa ya madini ya Nitrojeni na Fosforasi ambayo huhitajika kwa wingi kwenye chakula cha samaki.

Chanzo cha chakula kwa wafugaji: Pamoja na kuwa na umuhimu wa kiikolojia katika ufugaji mseto, lengo jingine kubwa ni kuwa chanzo cha lishe bora kwa mfugaji kwani huwa na protini ya kutosha ambayo husaidia katika ukuaji wa mwili.

Chanzo cha fedha: Kama ilivyo kwa mifugo wengine, mauzo yatokanayo na mazao kama kuku husaidia kama chanzo kikubwa cha fedha kuanzia wafugaji wadogo wadogo hadi wakubwa.

Kuku hufugwa kirahisi ukilinganisha na wanyama wakubwa kama vile ng'ombe, nguruwe, mbuzi na kondoo ambao huhitaji eneo kubwa, rasilimali kubwa, wasimamizi wengi, n.k.

Hivyo ufugaji wa kuku huwa na gharama ndogo kiuendeshaji na huleta faida kubwa.



# Kilimo cha migomba kina faida nyingi

**NCHINI Tanzania kilimo cha migomba kimekuwepo kwa miaka mingi. Kilimo hiki ni maarufu sana kwa sababu zao la ndizi limekuwa likitumika kama chakula kikuu kwa baadhi ya mikoa kama vile Kagera, Kilimanjaro na Mbeya.**



Zao la migomba limekuwa muhimu na kufuatiwa na mazao ya mahindi, mpunga, mtama, muhogo, viazi na mazao ya jamii ya kunde kama vile maharagwe.

Zao la ndizi linaweza kuwa moja kati ya mazao ya biashara iwapo litazalishwa kwa kufuata kanuni bora za uzalishaji wa zao hilo, ikiwa ni pamoja na kupanda aina bora ya migomba inayozaa ndizi zinazotambulika katika masoko ya kimataifa.

Nchini Tanzania mikoa inayoshughulika na kilimo cha migomba na kuzalisha zao la ndizi kwa wingi ni pamoja na Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Arusha, Manyara, Mara, Tanga, Morogoro, Kigoma na Pwani.

**MATUMIZI**

Kilimo cha migomba kina faida nyingi, baadhi ya faida za migomba na zao la ndizi ni: –

Zao la chakula na la biashara

Kutengenezea pombe pamoja na kulisha mifugo, kutengenezea mbolea (mboji), matandazwa shambani (mulch), kutoa kivuli, na kutoa nyuzi.

Kutengenezea vitu vya sanaa pamoja na kamba, malighafi ya kutengeneza vyakula na vinywaji mbalimbali, hutumika kutengenezea dawa, majani hutumika kama miamvuli, sahani, vikombe na kata na magome yake hutumika kuezekea.

**UZALISHAJI**

Zao la ndizi likizalishwa kwa utaalamu unaokubalika huweza kutoa mazao yenye ubora wa hali ya juu na kuongeza uzalishaji kwa eneo. Mambo yafuatayo yafaa kuzingatiwa katika uzalishaji wa zao hili.

**HALI YA HEWA**

Kiasi cha chini cha mvua kifaacho ni 100mm kwa mwezi au 1200mm kwa mwaka. Mwinuko ni kutoka usawa wa bahari hadi mita 1800 juu ya usawa wa bahari. Zaidi ya mwinuko huo migomba haikui vizuri.

Kiasi cha joto kinachofaa ni nyuzi joto za sentigredi 25 hadi 30 chini ya nyuzi joto 16 migomba haikui vizuri. Migomba hustawi vizuri kwenye udongo wenye rutuba ya kutosha, kina kirefu, usiotuamisha maji na pia usiwe na chumvi.

**AINA ZA NDIZI**

Kuna aina nyigi sana za ndizi. Nchini Tanzania ndizi zinazozalishwa, zipo za aina nyingi ambazo hutofautiana kwa majina kutokana na eneo au mkoa unaozalisha.

Hata hivyo zinaweza kugawanywa katika makundi mawili. Aina ambayo huliwa kwa kuzichoma, kukaanga au kupikwa zikichanganywa na vyakula vingine kama vile nyama. Aina za ndizi hizo ni pamoja na Mzuzu, Mshale, Matoke, Bokoboko na Mkono wa Tembo.

Aina nyingine ni zile ambazo huliwa kama matunda, aina hizo ni kama vile Kisukari, Kimalindi, Mzungu na Mtwike.

Kuna aina nyingine za ndizi ambazo kwa sasa huzalishwa hapa nchini ambazo zina fahamika kwa ubora wake katika masoko ya ndizi ya kimataifa. Aina hizi ni pamoja na Williams, Grand Naine, Pazz, Jamaica, Gold Finger, Nyingine ni Uganda green, Embwailuma Giant na Chinese Cavendish.

**UTAYARISHAJI WA SHAMBA**

Safisha sehemu inayohusika kwa kutumia zana ulizonazo.

Ng'oa visiki vyote na mizizi yake yote. Lima sehemu hiyo kwa kutumia jembe la mkono, rato, au trekta ili kuwezesha mizizi laini ya migomba kupenya ardhini kwa urahisi.

Baada ya visiki na magugu yote kuondolewa na hivyo ardhi kuwa wazi, uchimbaji wa mashimo ya kupandikiza machipukizi au miche ya migomba unaweza kufanyika.

Nafasi ya kuchimba mashimo

Mashimo yatachimbwa kwa nafasi inayokusudiwa kutumika kati ya mashina ya migomba na kati ya mistari kama ifuatavyo:-

Migomba inaweza kupandwa kwa nafasi ya umbali wa mita 2.75 kwa 2.75 kwa migomba mifupi kama Kimalindi na Kisukari.

Umbali wa mita 3 kwa mita 3 kwa migomba ya urefu wa kati kama Jamaica na Mshale.

Umbali wa meta 3.6 kwa meta 3.6 kwa migomba mirefu zaidi kama Uganda green.



# BART KUJIKUTA CHELSEA?



LONDON, England

**CHELSEA inamfuatilia kwa karibu kipa wa Uholanzi na klabu ya Brighton Bart Verbruggen, 22, kwa ajili ya uhamisho wa majira ya joto.**

Nazo Manchester United, Tottenham na Arsenal zimeonyesha nia ya kumsajili Benjamin Sesko kutoka RB Leipzig na mshambuliaji huyo wa Slovenia mwenye umri wa miaka 21 ana kipengele cha kutolewa ambacho kinaweza kutumika msimu huu wa joto.

## LIVERPOOL YAITWA KWA PEDRO



LONDON, England

**MSHAMBULIAJI wa Brighton wa Brazil Joao Pedro, 23, anataka kujiunga na Liverpool majira ya joto.**

Naye straika wa wa Canada Jonathan Davidyuko tayari kuondoka katika klabu hiyo kama mchezaji huru msimu huu wa joto.

## WHARTON JICHO LA MADRID

MADRID, Hispania

**WASAKA vipaji wa Real Madrid wamekuwa wakimfuatilia kiungo wa England Adam Wharton tangu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 arejee kwenye kikosi cha kwanza cha klabu ya Crystal Palace.**

Nayo Liverpool wameanza mazungumzo na Conor Bradley kuhusu kandarasi mpya ya miaka mitano ambayo itamuwezesha beki huyo wa Ireland Kaskazini, 21, kupata nyongeza ya 650%.

## JOHAN VASQUEZ MTU KATI

LONDON, England

**TIMU za Brentford na Fulham zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili beki wa Mexico Johan Vasquez, 26, kutoka Genoa.**

Fulham na Sporting wanamuwinda beki wa Ugiriki, Georgios Vagiannidis, huku Sporting wakiwasilisha dau la euro 10m (£8.3m) kwa Panathinaikos.

## PEP GUARDIOLA AJIPANGA

MANCHESTER, England

KOCHA wa Manchester City Pep Guardiola anatarajiwa kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa Uingereza Jack Grealish, 29, huku kukiwa na mipango ya kukimarisha kikosi cha City.

Inter Milan wanaibuka wapinzani wakuu wa Liverpool katika mbio za kumsajili kiungo wa Ujerumani Joshua Kimmich huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 akiingia akisalia na miezi michache katika mkataba wake na Bayern Munich.

Mjasiriamali spoti
JUMATANO MACHI 5, 2025
Tovuti: www.mjasiriamali.co.tz



# WANAPIGIKA TU!

## >> HUKO KOMBE LA SHIRIKISHO MAMBO YAMEZIDI KUWA MAZURI ZAIDI

NA MWANDISHI WETU

**HUKO Kombe la Shirikisho mnona wanapigika? Wenyeji, JKT Tanzania juzi walifanikiwa kutinga Hatua ya 16 Bora Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), michuano inayodhaminiwa na Benki ya CRDB baada ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Biashara United ya Mara Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni Jijini Dar es Salaam.**

Mabao ya JKT Tanzania yalifungwa na Shiza Kichuya dakika ya 19 na Najim Magulu dakika ya 47, wakati bao pekee la Biashara United lilifungwa na Freddy Kiwale dakika ya 82.

Nayo Tabora United ikaitupa nje Transit Camp kwa penalti 4-2 kufuatia sare ya kufungana bao 1-1 Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Mabingwa wa zamani wa michuano hiyo, Mtibwa Sugar wakaitupa nje Town Stars kwa kuichapa mabao 5-3 Uwanja w Manungu Complex, Morogoro.

Mechi nyingine za Hatua ya 32 Bora, Mbeya Kwanza iliichapa Mambali Ushirikiano mabao 3-0 Uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara.

Nao Songea United wakapata ushindi wa 1-0 ugenini dhidi ya Polisi Tanzania Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro, wakati Giraffe Academy waliilaz Green Warriors 1-0 Uwanja waUwanja wa Azimio mjini Katavi.

Ikumbukwe Jumapili Azam FC ilitupwa nje ya michuano hiyo baada ya kufungwa na Mbeya City kwa penalti 4-2 kufuatia sare ya 1-1 ndani ya dakika 90 - Mbeya wakianza kupata bao kupitia bao kupitia kwa Daniel William dakika ya 64, kabla ya kiungo Yahya Zaid kuisawazishia Azam FC dakika ya 90'+5.

# CHAMA APEWA FAGIO LAKE

NA MWANDISHI WETU

**ERASTO Nyoni kiraka anayetimiza majukumu yake ndani ya kikosi cha Namungo kinachonolewa na Kocha Mkuu, Juma Mgunda ameweka wazi kuwa nyota Clatous Chama amebadilika hasa kwenye upande wa spidi ila watu wanamtazama kwa mazoea.**

Ipo wazi kwamba Chama ni mchezaji wa kwanza kutambulishwa ndani ya kikosi cha Yanga kwenye dirisha kubwa la usajili ilikuwa ni Julai Mosi 2024 ambapo aliibuka hapo akiwa ni mchezaji huru baada ya kumaliza kandarasi yake ndani ya kikosi cha Simba.

Chama alipokuwa Simba alikuwa chaguo la kwanza lakini kwa sasa ndani ya kikosi cha Yanga ambacho kwenye anga la kimataifa kimegotea hatua ya makundi sio chaguo la kwanza amekuwa akipokezana namba na Aziz Ki ambaye naye ni kiungo mshambuliaji wakati mwingine Pacome.

Nyoni aliwahi kucheza na Chama katika kikosi cha Simba kabla ya kukutana na Thank You na sasa anaendelea kutimiza majukumu ndani ya Namungo ambayo Februari 27 2025 ilishuhudia ubao wa Uwanja wa Azam Complex ukisoma Azam FC 1-1 Namungo.

Kiungo huyo amesema: "Chama amebadilika kwenye suala zima la uchezaji ila kwa kuwa yupo kwenye timu mpya watu wanamuangalia kwa mazoea tu ninaweza kusema hivyo. Ukimuangalia kwenye uchezaji wake ameongezeka spidi lakini kuna watu hawawezi kujua.

## MZEE BABA — SHEDRACK KILASI

